TANGAZO LA SERIKALI NA. 444 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 22(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI RONDO YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi Rondo ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la hifadhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi Rondo.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA LINDI

MSITU WA HIFADHI RONDO

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 2979.10 au Kilometa za Mraba 29.79 Unakopatikana na Mipaka Eneo lote la ardhi iliyohifadhiwa awali chini ya Msitu wa Hifadhi Rondo bila kujumuisha eneo la Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Rondo linalopatikana Wilaya ya Lindi, Mkoa wa Lindi kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2865 ya mwaka 2014 (Skeli 1:10,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo La Serikali Na. 444 (Linaendelea)*




Dodoma,
__24 May, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI
*Waziri wa Maliasili na Utalii*